GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXXI Nam. 6974 **18 Febuari, 2022** **Bei, Shs.4500**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mapato yatokanayo na Uhalifu Nam. 10 ya 2009. 90

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mapato yatokanayo na Uhalifu Nam. 10 ya 2009.

TANGAZO

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanzia tarehe 16 Februari, 2022 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza, pili na tatu na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
2 Februari, 2022

(Mhandisi Zena Ahmed Said)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika anyumba ya kupiga, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA
wa
SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA UDHIBITI WA FEDHA HARAMU NA MAPATO YATOKANAYO NA UHALIFU NAM. 10 YA 2009

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mapato yatokanayo na Uhalifu, 2022 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Kusomwa.

2. Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mapato yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009, ambayo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria Mama".

SEHEMU YA PILI
VIFUNGU VYA MAREKEBISHO

Marekebisho ya kifungu cha 2.

3. Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza tafsiri mpya ya maneno kwa mpangilio wake wa kialfabeti kama ifuatavyo:

"Benki" ina maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania;

"hati ya malipo ya mmiliki" maana yake ni hati ya malipo ya fedha katika mfumo wa mmiliki kama vile:

(a) hundi ya msafiri;

(b) hati za malipo ikijumuisha hundi, hati ya ahadi ya malipo na hawala za fedha ambazo zipo katika mfumo wa mmiliki, imeidhinishwa bila ya vikwazo, iliyofanywa kwa mlipwaji asiyetambulika au katika mfumo ambao jina la hati linapitishwa wakati wa kulipwa;

(c) hati za malipo ambazo hazijakamilika kama vile, hundi, hati za ahadi ya malipo na hawala za fedha zilizosainiwa, lakini jina la anayelipwa halijatajwa;

"umiliki wa hisa zisizosajiliwa" maana yake ni hati za malipo zinazotoa umiliki kwa mtu mwenye utu wa kisheria kwenda kwa mtu anayemiliki cheti cha umiliki wa hisa zisizosajiliwa;

"mmiliki mnufaika" maana yake ni mtu binafsi ambaye anammiliki au anamdhibiti mteja, mtu binafsi ambaye kwa niaba yake muamala au shughuli inafanywa, mtu ambaye anadhibiti kikamilifu taasisi inayojitegemea au mnufaika wa bima au mnufaika wa uwekezaji katika bima na inajumuisha watu binafsi kama watakavyotambuliwa chini ya kifungu cha 10B;

"uhusiano wa kibiashara" maana yake ni utaratibu wa kibiashara au kitaaluma baina ya mtoa taarifa na mteja ambao unahusisha kuweka utaratibu maalum wa akaunti ya mteja pale ambapo miamala inafanyika mara kwa mara, kimazowea au kikawaida;

"mamlaka zenye uwezo" maana yake ni chombo cha umma chenye dhamana ya kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi au ufadhili wa silaha za maangamizi ikijumuisha taasisi ya usimamizi, mamlaka ya forodha, chombo cha kusimamia utekelezaji wa sheria, Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU), Kamati ya Kitaifa ya Wataalam ya Kudhibiti Fedha Haramu na taasisi ya usajili au utoaji wa leseni;

"mteja" maana yake ni mtu binafsi au mtu mwenye utu wa kisheria, au utaratibu wa kisheria ambapo mteja hupokea bidhaa au huduma toka kwa mtoa taarifa kwa malipo ya fedha au malipo ya aina nyengine yoyote;

"utambuzi wa mteja" inajumuisha kumtambua mteja, mmiliki mnufaika au mtu anayedai kuwa anamuwakilisha mteja, na:

(a) kwa upande wa mteja, kufanya baadhi au yote kati ya yafuatayo, kulingana na utambuzi wa viashiria hatarishi vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi au ufadhili wa silaha za maangamizi:

(i) kuhakiki utambulisho wa mteja kwa kutumia vyanzo vya nyaraka, data au taarifa zinazoaminika na zinazojitegemea;

(ii) kufahamu na itakapoonekana inafaa kupata taarifa zinazohitajika kuhusu aina na madhumuni ya uhusiano wa kibiashara;

(iii) kufahamu kazi ya mteja;

(iv) kufahamu umiliki na mfumo wa udhibiti wa mteja;

(v) kuhakikisha chanzo cha mapato na fedha za mteja;

(vi) kutambua utambulisho wa wamiliki wanufaika na kuchukua hatua stahiki kuhakiki utambulisho wao kwa kutumia vyanzo vya nyaraka, data au taarifa zinazoaminika na zinazojitegemea; na

(vii) kuhakikisha kwamba mtu yeyote anayedai kuwa anamuwakilisha mteja kuwa ameidhinishwa na kutambua na kuhakiki utambulisho wa mtu huyo kwa kutumia vyanzo vya nyaraka, data au taarifa zinazoaminika na zinazojitegemea;

(b) kwa upande wa mmiliki mnufaika, kufanya baadhi au yote kati ya yafuatayo, kulingana na utambuzi wa viashiria hatarishi vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi au ufadhili wa silaha za maangamizi:

(i) kuchukua hatua stahiki kuhakiki utambulisho wa mmiliki mnufaika kwa kutumia vyanzo vya nyaraka, data au taarifa zinazoaminika na zinazojitegemea;

(ii) kufahamu kazi ya mmiliki mnufaika;

(iii) kuhakikisha chanzo cha mapato na fedha za mmiliki mnufaika;

(c) kwa upande wa mtu anayedai kuwa anamuwakilisha mteja, kufanya baadhi au yote kati ya yafuatayo, kulingana na utambuzi wa viashiria hatarishi vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi au ufadhili wa silaha za maangamizi:

(i) kuhakiki utambulisho wa mtu huyo kwa kutumia vyanzo vya nyaraka, data au taarifa zinazoaminika na zinazojitegemea;

(ii) kufahamu kazi ya mtu huyo;

(iii) kufahamu uhusiano kati ya mtu huyo na mteja; na

(iv) kuhakikisha kuwa mtu huyo ameidhinishwa kumuwakilisha mteja;

"fedha" maana yake ni mali ya kila aina, inayoonekana na isiyoonekana, inayoshikika na isiyoshikika, inayohamishika na isiyohamishika, nyaraka au hati za kisheria katika mfumo wowote bila ya kujali namna zilivyopatikana, ikijumuisha njia za kielektroniki au wa kidigitali, zinazothibitisha umiliki au maslahi katika mali husika;

"taasisi ya kifedha" maana yake ni mtu yeyote ambaye anafanya biashara katika moja au zaidi ya shughuli zifuatazo:

(a) kupokea amana au fedha ambazo hurejeshwa kwa mwekaji kutoka benki ya umma au benki ya binafsi na fedha nyengine ambazo hurejeshwa kwa kutumia njia za malipo ya umma, inayotoa au inayosimamia, inayofanya biashara ya kubadilisha fedha za nje au dhamana zinazohamishika au kubadilisha sarafu za kimtandao, watoa huduma pochi, wanaofanya taratibu za malipo au watumaji, na mifumo mengine ya biashara ya sarafu za kimtandao;

(b) kukopesha ikijumuisha mkopo wa kawaida, mkopo wa nyumba, mikopo inayotokana na madai, kufadhili miamala ya kibiashara ikijumuisha kutaifisha mali;

(c) mikopo kwa njia ya kukodisha mali;

(d) dhamana na mikopo ya nyumba;

(e) huduma za kutuma fedha au thamani, pasipo kuhusisha watoa huduma za kuendesha mitambo na kutuma ujumbe au mifumo mengine wezeshi katika kutuma fedha;

(f) kutoa na kusimamia njia za malipo ikijumuisha kadi za mikopo, kadi za benki, hundi za benki, hawala za fedha, hundi, hundi za msafiri, fedha, hati ya malipo ya biashara ya benki, fedha za kielektroniki;

(g) dhamana za fedha;

(h) biashara ya dhahabu;

(i) biashara ya:

(i) hati za soko la fedha ikijumuisha hundi, bili, cheti cha amana, dhamana ya kifedha;

(ii) kubadili fedha za kigeni;

(iii) kubadilishana, kiwango cha riba na hati za orodha;

(iv) dhamana zinazohamishika; na

(v) bidhaa ya biashara ya baadaye;

(j) biashara ya dhamana, udalali wa dhamana na ushiriki katika soko la dhamana;

(k) uwekezaji wa mtu binafsi na uwekezaji wa pamoja;

(l) udhamini na usimamizi wa mifumo ya uwekezaji wa pamoja;

(m) utunzaji na usimamizi wa fedha taslim au dhamana za kubadilika kiurahisi kwa niaba ya watu wengine;

(n) kuwekeza, kusimamia fedha kwa niaba ya watu wengine;

(o) usimamizi wa mfuko wa pensheni;

(p) bima, uwakala wa bima au udalali; na

(q) ubadilishaji wa fedha na sarafu;

"utaratibu wa kisheria" maana yake ni amana au taratibu nyengine zinazofanana na hizo;

"afisa mtoa taarifa za utakatishaji wa fedha haramu" maana yake ni mtu binafsi aliyeajiriwa au vyenginevyo amehusishwa na mtoa taarifa kupokea taarifa za waajiriwa wa mtoa taarifa kuhusiana na shughuli ambazo zinaweza kupelekea utakatishaji wa fedha haramu;

"muamala wa nadra" maana yake ni ubadilishanaji baina ya mtoa taarifa ambaye anatoa bidhaa au huduma na mteja ambaye analipia bidhaa au huduma kwa njia ya fedha au kwa malipo mengine yoyote ambapo ubadilishanaji huo unafanywa nje ya uhusiano wa kibiashara;

"mtu mwenye wadhifa maalum" maana yake ni mtu binafsi aliyepewa dhamana kubwa katika umma, ndani au nje ya nchi, au mtu binafsi aliyepewa dhamana kubwa na shirika la kimataifa, mtu huyo inajumuisha wanafamilia na washirika wake wa karibu;

"ufadhili wa silaha za maangamizi" maana yake ni kitendo kinachofanywa na mtu yeyote ambaye kwa namna yoyote, moja kwa moja au vyengineyo, anatoa msaada au anatoa mali yote au sehemu ya mali, fedha, rasilimali za kiuchumi, teknolojia au huduma kwa ufadhli wowote wa silaha za maangamizi, au kwa mtu yeyote, au mamlaka au kwa manufaa ya mtu yeyote aliyetajwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa chini ya Sura VII ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa (kwa mujibu wa maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ambayo yanahusiana katika kuzuia na kutokomeza ufadhili wa silaha za maangamizi), kwa ajili ya kupata, kumiliki, kufanya udalali, kutengeneza, kuendeleza, kuhifadhi, kusafirisha, kuhamisha, kuhaulisha, kuingiza au kutoa nje ya nchi, silaha za nyuklia, kemikali au za kibaiolojia au kutumia bidhaa zenye matumizi ya aina mbili, nyenzo zake za kuwezesha silaha hizo kutumika au vifaa vinavyohusiana navyo;

"hatua stahiki" maana yake ni hatua muafaka zinazoendana na viashiria hatarishi vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi au ufadhili wa silaha za maangamizi;

"tathmini ya viashiria hatarishi" maana yake ni kutambua, kutathmini na kufahamu viashiria hatarishi;

"uongozi wa juu" maana yake ni watu binafsi ndani ya chombo kinachojitegemea walio katika ngazi ya juu ya uongozi na wenye dhamana ya kusimamia majukumu ya kila siku katika chombo hicho kinachojitegemea;

"amana na mtoa huduma za kampuni" maana yake ni mtu yeyote, isipokuwa mamlaka za usajili na utoaji wa leseni, ambaye kupitia shughuli zake, anatoa moja kati ya huduma zifuatazo:

(a) uanzishwaji wa vyombo vinavojitegemea;

(b) kuwa au kumuandaa mtu mwengine kuwa, mkurugenzi, katibu au nafasi inayofanana na hiyo kuhusiana na chombo kinachojitegemea;

(c) kuipatia ofisi iliyosajiliwa, anuani za biashara, za mawasiliano au anuani kwa ajili ya uendeshaji na huduma nyengine zinazohusiana na vyombo vinavyojitegemea;

(d) kuwa au kumuandaa mtu mwengine kuwa, mdhamini wa amana au utaratibu mwengine wa kisheria unaofanana;

(e) kuwa au kumuandaa mtu mwengine kuwa, mwenye hisa aliyeteuliwa kwa niaba ya mtu mwengine asiyekuwa kampuni iliyoorodheshwa katika soko linalosimamiwa ambalo linawajibu wa kutoa vigezo kwa mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vinavyolingana;

"mali za kimtandao" maana yake ni uwakilishi wa mali kidijitali inayoweza kufanyiwa biashara, kuhamishwa, kufanya malipo au kuwekeza kwa njia ya mtandao na inayotambuliwa na Serikali lakini haijumuishi uwakilishi wa kidijitali wa sarafu za kawaida, dhamana na mali nyenginezo za kifedha ambazo tayari zinatumika katika sheria za Zanzibar;

"mtoa huduma wa mali za kimtandao" maana yake ni mtu yeyote anayefanya moja au zaidi ya shughuli zifuatazo kwa ajili ya au kwa niaba ya mteja:

(a) kubadili kati ya mali za kimtandao na mali za kawaida;

(b) kubadili kutoka aina moja ya mali za kimtandao kwenda nyengine;

(c) kuhamisha mali za kimtandao;

(d) kutunza au kusimamia mali za kimtandao au nyenzo zinazowezesha udhibiti wa mali za kimtandao; na

(e) kushiriki katika utoaji wa huduma za kifedha zinazohusiana na mtoa ahadi au mauzo ya mali za mtandao.

(b) kufuta maana ya maneno "kosa kubwa", "benki", "chombo cha kusimamia utekelezaji wa sheria", "taasisi ya usimamizi", "mtoa taarifa", "ofisa wa polisi" na "kosa maalum" na kuweka badala yake maana ya mapya yafuatayo:

"benki" ina maana kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha;

"chombo cha kusimamia utekelezaji wa sheria" maana yake ni Jeshi la Polisi Tanzania, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Idara ya Uhamiaji Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Bodi ya Mapato Zanzibar, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar na mamlaka nyengine yoyote iliyoindhinishwa kufanya uchunguzi wa makosa ya jinai;

"ofisa mchunguzi" maana yake ni mjumbe wa Jeshi la Polisi au mwenye cheo cha kuanzia koplo kwenda juu na ofisa mwengine yeyote aliyeidhinishwa na sheria husika kufanya uchunguzi wa jinai;

"taasisi ya usimamizi" inajumuisha:

(a) Benki Kuu ya Tanzania;

(b) Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania;

(c) Mrajis wa Vyama vya Ushirika;

(d) Mrajis wa Jumuiya;

(e) Msajili wa Vyama vya Siasa;

(f) Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar;

(g) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania;

(h) Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar;

(i) Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar; na

(j) mamlaka nyengine zozote za usimamizi au wakala ambao, Waziri anaweza kuutangaza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali;

"mtoa taarifa" maana yake ni:

(a) taasisi ya fedha;

(b) wakala wa majengo, mhasibu, mkaguzi wa hesabu, mshauri wa kodi, muuzaji wa kazi za sanaa;

(c) muuzaji wa madini na vito vya thamani;

(d) wakili, msimamizi wa viapo na mtaalamu mwengine wa kisheria anayejitegemea endapo:

(i) anamsaidia mteja kuandaa na kutekeleza miamala inayohusu:

(aa) kununua au kuuza nyumba au viwanja au majengo ya kibiashara;

(bb) kusimamia na kuratibu fedha, dhamana au mali nyengine yoyote ya mteja;

(cc) kufungua au kusimamia akaunti za benki, akaunti za akiba au akaunti nyengine;

(dd) kuratibu michango inayohitajika kuanzisha, kusimamia au kuyaelekeza mashirika au taasisi;

(ee) uanzishwaji, usimamizi au muongozo wa mashirika au taasisi; na

(ff) ununuzi au uuzaji wa taasisi za kibiashara;

(ii) kumuwakilisha mteja katika miamala ya fedha au majengo;

(e) mwendesha mnada;

(f) amana na mtoa huduma za kampuni;

(g) ofisi ya kutunza taarifa za wakopaji;

(h) muuzaji wa vyombo vya moto;

(i) wakala wa forodha; na

(j) mtu mwengine yeyote ambaye Waziri atamtangaza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali;

"kosa kubwa" maana yake ni kosa dhidi ya sheria yoyote Zanzibar au katika nchi ya kigeni kwa tendo ambalo lingefanyika Zanzibar, lingekuwa kosa kubwa ambapo adhabu yake ni kifo au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na mbili, na linajumuisha kosa jengine lolote ambapo mali imetumika au mapato yaliyopatikana au faida zilizopatikana;

"kosa maalum" maana yake ni kosa kubwa.

Kufuta na kuweka badala yake kichwa cha habari kipya cha Sehemu ya III.

4. Kichwa cha habari cha Sehemu ya III cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kichwa cha habari kipya kama ifuatavyo:

"SEHEMU YA III
USIMAMIZI WA UDHIBITI WA UTAKATISHAJI WA FEDHA HARAMU, UFADHILI WA UGAIDI NA UFADHILI WA SILAHA ZA MAANGAMIZI"

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 10.

5. Kifungu cha 10 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 10 kama ifuatavyo:

"Kufanya tathmini ya viashiria hatarishi.

10.-(1) Tathmini za viashiria hatarishi vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi zitafanywa Zanzibar.

(2) Tathmini za viashiria hatarishi zitajumuisha kutambua, kufanya tathmini na kufahamu viashiria hatarishi katika ngazi ya taifa, sekta na taasisi na kutumia njia sahihi za kudhibiti viashiria hatarishi.

(3) Tathmini ya viashiria hatarishi zitafanywa na mamlaka zenye uwezo na watoa taarifa katika udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi na kuidhinishwa na uongozi wa juu.

(4) Katika kufanya tathmini ya viashiria hatarishi, mtu au taasisi inaweza kuomba msaada, data au taarifa kutoka kwa mtu yeyote ndani au nje ya Zanzibar.

(5) Kutakuwa na taratibu za kutoa na kubadilishana taarifa miongoni mwa wadau husika, zinazotokana na tathmini ya viashiria hatarishi kwa ajili ya kujenga uelewa kwa:

(a) kuweka vipaumbele juu ya mgawanyo wa rasilimali;

(b) kusaidia katika kupunguza viashiria hatarishi vinavyohusiana; na

(c) kusaidia kuanza utekelezaji wa mikakati bora ya kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.

(6) Watoa taarifa watafanya tathmini ya viashiria hatarishi vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi inayohusiana na:

(a) wateja wapya na waliopo, nchi au maeneo ya kijiografia, bidhaa, huduma, miamala na njia zinazotumika kutoa huduma;

(b) bidhaa mpya au zinazoendelezwa, shughuli za biashara, huduma, teknolojia na njia zinazotumika kabla ya kuzinduliwa au kutumiwa;

(c) bidhaa zilizopo, shughuli za biashara, huduma, teknolojia, na njia zinazotumika kutoa huduma, ambazo zimefanyiwa mabadiliko, kabla ya kuendelea kutumiwa; na

(d) matumizi ya teknolojia mpya au teknolojia zinazoendelea kwa bidhaa mpya na zilizokuwepo kabla.

(7) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (6) cha aya (d) cha kifungu hiki, bidhaa mpya zitajumuisha uhaulishaji wowote ndani ya sarafu za kimtandao au mitandao ya mali iliyogatuliwa, uhamishaji wa mtu hadi mtu mwengine unaohusisha watoaji na wamiliki wa huduma pochi, malipo makubwa ya sarafu za kimtandao au uhamishaji wa mali, malipo ya simu na huduma za malipo za kimtandao.

(8) Kwa kuzingatia Sheria yoyote husika inayoruhusu kutumika sarafu za kimtandao au mali, wakati wa kufanya tathmini ya viashiria hatarishi kuhusiana na sarafu za kimtandao au mali za kimtandao, watoa taarifa wazingatie viashiria vilivyobainika kutokana na ujumbe au sehemu za makutano ambazo hutumika kuhamisha thamani ndani na nje ya sarafu za kawaida na wachukue hatua madhubuti za kutambua hatari kubwa ya sarafu za kimtandao au mali za kimtandao zinazoweza kubadilishwa.

(9) Watoa taarifa watakuwa na utaratibu maalum wa kutoa majibu, matokeo na taarifa nyengine kwa mamlaka zenye uwezo, juu ya tathmini ya viashiria hatarishi iliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (6) cha kifungu hiki.

(10) Mamlaka zenye uwezo na watoa taarifa:

(a) wanatakiwa wawe na sera zilizoandikwa, udhibiti na taratibu ambazo zimeidhinishwa na uongozi wa juu ili kusimamia na kupunguza viashiria hatarishi vilivyobainika chini ya vifungu vidogo vya (1) na (6) vya kifungu hiki;

(b) wahakikishe kiwango cha taarifa za kina za sera zilizoandikwa, udhibiti na taratibu kwa upande wa watoa taarifa zinaendana na ukubwa, muundo na changamoto za shughuli ya mtoa taarifa;

(c) wafuatilie na wakague utekelezaji wa sera, udhibiti na taratibu;

(d) wafanye mapitio mara kwa mara na kuhuisha sera, udhibiti na taratibu na kutunza kumbukumbu za mapitio na mabadiliko hayo; na

(e) wachukue tahadhari za ziada ili kudhibiti viashiria hatarishi endapo kutabainika kiwango kikubwa cha viashiria hatarishi.

(11) Tathmini ya viashiria hatarishi iliyoelezwa chini ya vifungu vidogo vya (1) na (6) itawekwa kwenye maandishi na kuhuishwa ili iendane na wakati na mabadiliko ya viashiria hatarishi angalau mara moja kwa mwaka.

(12) Kitengo cha Udhibiti Fedha Haramu au Taasisi ya usimamizi zitatoa muongozo kwa mamlaka zenye uwezo na watoa taarifa katika kufanya tathmini ya viashiria hatarishi juu ya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.”

Kuongeza vifungu vipya vya 10A, 10B na 10C.

6. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 10A, 10B na 10C mara baada ya kifungu cha 10 kama ifuatavyo:

“Udhibiti wa viashiria hatarishi na kutenga rasilimali kulingana na viashiria hatarishi.

10A. Kwa kuzingatia viashiria hatarishi vilivyoainishwa chini ya kifungu cha 10:

(a) taasisi ya usimamzi itafuatilia ipasavyo watoa taarifa waliopo chini yake na kuchukuwa hatua za lazima ili kuhakikisha viashiria hatarishi vinadhibitiwa, vinapunguzwa na kuhakikisha utekelezaji wa masharti ya udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi yanafuatwa;

(b) mamlaka zenye uwezo na watoa taarifa wanaweza kutumia njia nyepesi katika udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi, panapothibitika uwepo wa kiwango cha chini cha viashiria hatarishi vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi;

(c) mamlaka zenye uwezo na watoa taarifa wanaweza kutumia njia nyepesi kudhibiti na kupunguza viashiria hatarishi, ikiwa tathmini za viashiria hatarishi zinaonesha maeneo yenye hatari ndogo na hakuna mashaka ya kuwepo utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi;

(d) njia za kudhibiti zinazotumika ziendane na viashiria hatarishi vilivyobainika na mamlaka zenye uwezo na watoa taarifa watoe maelezo wenyewe juu ya ulinganifu wake na viashiria hatarishi au watapotakiwa na Mamlaka husika."

"Utambuzi wa mmiliki mnufaika.

10B. Mtu atatambulika kuwa ni mmiliki mnufaika endapo:

(a) ikiwa mteja ni chombo chenye utu wa kisheria:

(i) mtu binafsi ambaye moja kwa moja au vyenginevyo anamiliki au kudhibiti chombo chenye utu wa kisheria kupitia umiliki wa kiasi cha hisa au maslahi ya kutosha au kuwa na haki ya kupiga kura, au maslahi katika umiliki katika chombo chenye utu wa kisheria na umiliki huo, maslahi katika umiliki au udhibiti na inajumuisha, kumiliki hisa zisizosajiliwa, kuwa na uwezo wa kuteua au kuondoa wajumbe wengi wa bodi, afisa mtendaji mkuu au uongozi wa juu;

(ii) umiliki wa asilimia tano au zaidi wa hisa katika chombo chenye utu kisheria, au maslahi katika umiliki wa asilimia tano au zaidi wa hisa katika chombo chenye utu kisheria zinazomilikiwa na mtu binafsi itakuwa ni ishara ya mtu huyo kuwa na umiliki wa moja kwa moja au asilimia ya kutosha ya hisa au haki ya kupiga kura au maslahi katika umiliki katika chombo hicho chenye utu wa kisheria au umiliki wa asilimia tano au zaidi wa hisa au maslahi katika umiliki wa asilimia tano katika chombo chenye utu kisheria inayomilikiwa na chombo chenye utu kisheria, ambazo zipo chini ya mamlaka ya mtu binafsi, au inamilikiwa na vyombo vyenye utu kisheria, ambazo zipo chini ya mamlaka ya mtu huyo huyo, itakuwa ni ishara ya kuwa na umiliki usiokuwa wa moja kwa moja;

(iii) endapo, baada ya kutumia njia zote zinazowezekana na bado hakuna sababu za kushuku utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi, na hakuna mtu binafsi chini ya aya ndogo ya (i) aliyeainishwa, au iwapo kuna shaka kuwa mtu aliyeainishwa ni mmiliki mnufaika, mtu binafsi anaeshikilia nafasi ya juu ya uongozi kwenye chombo hicho chenye utu kisheria atachukuliwa kuwa mmiliki mnufaika;

(b) ikiwa mteja ni amana:

(i) mlowezi, mdhamini au msimamizi;

(ii) wanufaika, au ikiwa mtu binafsi anayenufaika kutokana na amana bado hajatambuliwa, makundi ya watu binafsi wanaolengwa na madhumuni makuu ya kuanzishwa kwake yamewekwa au yanafanya kazi; na

(iii) mtu mwengine yeyote atakayedhibiti amana kwa njia ya umiliki wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja au vinginevyo;

(c) ikiwa mteja ni chombo chengine kilichoanzishwa kwa utaratibu wa kisheria, mtu binafsi mwenye kumiliki nafasi inayolingana au iliyosawa na nafasi zilizoelezwa katika aya ya (b);"

"Mtoa taarifa kutambua mteja.

10C.-(1) Mtoa taarifa:

(a) atawajibika kumtambua mteja kwa mujibu wa viashiria hatarishi vilivyobainika:

(i) kabla ya kuanzisha uhusiano wa kibiashara;

(ii) kabla ya kufanya muamala wa nadra;

(iii) endapo kutakuwa na shaka ya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi au ufadhili wa silaha za maangamizi;

(iv) ikiwa ukweli au usahihi wa nyaraka, data au taarifa zilizopatikana awali kwa madhumuni ya kumtambua mteja unatiliwa shaka; au

(v) kwa kuzingatia uzito wa viashiria hatarishi vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi au ufadhili wa silaha za maangamizi;

(b) ataendelea kufanya utambuzi wa mteja, baada ya kuanzisha uhusiano wa kibiashara, ikijumuisha kuhuisha taarifa za mteja;

(c) asifungue au asishughulikie akaunti iliyofunguliwa kwa jina la bandia, la uongo, lisilofahamika, lisilojulikana, la kificho au la kubuni;

(d) asianzishe uhusiano wa kibiashara, ikiwa haiwezekani kukamilisha utambuzi wa mteja, isipokua itakapothibitika uwepo wa hatari ndogo, uhusiano wa kibiashara unaruhusiwa kuanza;

(e) atasitisha uhusiano uliopo wa kibiashara, endapo itashindikana kukamilisha utambuzi wa mteja; na

(f) atawasilisha kwa FIU taarifa ya muamala shuku, iwapo itashindikana kukamilisha utambuzi wa mteja, kwa mujibu wa aya za (d) na (e) ya kifungu hiki kidogo.

(2) Katika mazingira ya kumtambua mtu mwenye wadhifa maalum, mtoa taarifa atafanya utambuzi kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na:

(a) awe na mifumo maalum ya kusimamia viashiria hatararishi ili kutambua kama mteja ni mtu mwenye wadhifa maalum;

(b) apate idhini ya uongozi wa juu kwa ajili ya kuanzisha uhusiano wa kibiashara na mteja huyo;

(c) achukue hatua stahiki kubaini chanzo cha mali na fedha; na

(d) aendelee kufuatilia kwa kina uhusiano huo.”

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 11.

7. Kifungu cha 11 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 11:

“Watoa taarifa kuanzisha na kutunza kumbukumbu za mteja.

11.-(1) Kila mtoa taarifa ataanzisha na kutunza kumbukumbu zote za:

(a) miamala ya kitaifa na kimataifa;

(b) taarifa za utambuzi wa mteja;

(c) taarifa za akaunti ya mteja;

(d) mawasiliano ya kibiashara;

(e) tathmini za viashiria hatarishi vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi;

(f) matokeo ya uchambuzi uliofanywa katika udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi; na

(g) taarifa za miamala shuku, taarifa nyengine na takwimu zinazohitajika kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Kila mtoa taarifa atatunza kumbukumbu zinazohitajika chini ya kifungu hiki kwa muda usiopungua miaka mitano tokea tarehe ambapo:

(a) shughuli zote zinazohusiana na muamala au miamala yenye uhusiano ilipokamilika au ilipofanyiwa kazi kwa mara ya mwisho;

(b) uhusiano wa kibiashara ulipositishwa rasmi;

(c) uchambuzi ulipokamilika; au

(d) tathmini ya viashiria hatarishi vya utakatishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi au ufadhili wa silaha za maangamizi ilipokamilika.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, mtoa taarifa atatunza kumbukumbu zote kwa muda utakaotakiwa na mamlaka yenye uwezo endapo ripoti imewasilishwa FIU au mtoa taarifa anaamini kwamba suala husika lipo chini ya uchunguzi.

(4) Kumbukumbu zinazohitajika chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zitajumuisha maelezo yanayojitosheleza ya kuainisha:

(a) jina kamili, kazi na anuwani itakapohitajika, biashara au shughuli kuu ya mteja au ya kila mtu anayefanya muamala au mtu ambae muamala umefanywa kwa niaba yake au njia iliyotumiwa na mtoa taarifa kuhakiki utambulisho wa kila mtu;

(b) uhalisia na tarehe ya muamala;

(c) aina na kiwango cha fedha husika;

(d) aina na nambari ya utambulisho wa akaunti yoyote pamoja na mtoa taarifa aliyehusika katika muamala;

(e) endapo muamala unahusisha hati ya malipo:

(i) jina la mlipaji;

(ii) jina la taasisi ambapo hati ya malipo imetoka;

(iii) jina la mlipwaji, kama lipo;

(iv) kiwango cha fedha na tarehe ya hati ya malipo;

(v) nambari ya utambulisho ya hati ya malipo, kama ipo; na

(vi) maelezo yoyote yanayotoa ridhaa yanayoonekana kwenye hati;

(f) jina na inapohitajika anwani ya mtoa taarifa, na ya Ofisa, mfanyakazi au wakala wa mtoa taarifa aliyeandaa kumbukumbu.

(5) Kumbukumbu zilizotunzwa kwa mujibu ya kifungu hiki zitatolewa kwa wakati kwa mamlaka zenye uwezo endapo zitakapoombwa.

(6) Endapo mtoa taarifa atahitajika kutoa nyaraka yoyote chini ya kifungu hiki, atabakia na nakala ya nyaraka hiyo na atatunza daftari la kumbukumbu la nyaraka zilizotolewa likiwa na maelezo kama itakavyoainishwa katika kanuni.

(7) Mtoa taarifa yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atapewa adhabu za kiutawala kwa mujibu wa kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii au adhabu kwa makosa ya jinai kwa mujibu wa kifungu cha 14 cha Sheria hii.”

8. Kifungu cha 12 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa: Marekebisho ya Kifungu cha 12.

(a) kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

“(1) Endapo mtoa taarifa anashuku au ana sababu za msingi za kushuku kwamba, fedha au mali ni mapato yatokanayo na uhalifu, au yanahusiana au yanahusishwa au yatatumika kutenda au kuendeleza kosa maalum au ana ufahamu wa ukweli au shughuli inayoweza kuwa dalili ya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi, ufadhili wa silaha za maangamizi au kosa maalum, ndani ya masaa ishirini na nne baada ya kupata mashaka, na ikiwezekana kabla ya kufanywa kwa muamala wowote:

(a) achukue hatua stahiki ili kujua madhumuni ya fedha au mali, muamala au muamala unaopendekezwa au unaotarajiwa, chanzo na mwisho wa fedha au mali inayohusika, na utambulisho na anwani ya mnufaika yeyote wa mwisho; na

(b) kuandaa ripoti ya muamala, au muamala unaopendekezwa au unaotarajiwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), na awasilishe ripoti hiyo FIU kwa njia yoyote salama kama itakavyoelezwa na FIU.”

(b) kuingiza maneno “ametenda kosa na” baada ya maneno “kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki” yanayojitokeza katika kifungu kidogo cha (4).

(c) kuingiza maneno “faini isiyopungua Milioni Moja au” baina ya maneno “atalipa” na “kifungo” yanayojitokeza katika aya ya (a) ya kifungu kidogo cha (4).

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 13.

9. Kifungu cha 13 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 13 kama ifuatavyo:

“Watoa taarifa kuanzisha na kutunza taratibu za ndani za kuripoti.

13.-(1) Mtoa taarifa ataanzisha na kutunza sera za ndani, taratibu na udhibiti ambao:

(a) utahakikisha kwamba watu watakaohusishwa au kuajiriwa na mtoa taarifa wanachunguzwa kikamilifu na kuhakikiwa kwa ajili ya kuajiri watu wenye sifa na uadilifu;

(b) utamteua mtu binafsi katika uongozi wa juu kama Afisa mtoa taarifa katika utakatishaji wa fedha haramu, ambaye waajiriwa wake watatoa taarifa za shuku au miamala yoyote inayohusiana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi, ufadhili wa silaha za maangamizi au shughuli ya kijinai yoyote ambayo waajiriwa wataitambua katika kutekeleza kazi zao;

(c) utamuwezesha Afisa mtoa taarifa wa utakatishaji wa fedha haramu kupata taarifa stahiki ambazo zinaweza kuhusika katika kutambua iwapo vigezo vya kujitosheleza vipo vya kuripoti shughuli au muamala shuku kwa FIU, kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha sheria hii;

(d) utamtaka mtoa taarifa wa utakatishaji wa fedha haramu kutoa taarifa FIU za shughuli au muamala shuku kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria hii, endapo kutakuwa na sababu za msingi za kulitolea taarifa jambo hilo;

(e) utaweka njia za kuhakikisha waajiriwa wanatambua sheria inyohusiana na kupambana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi, na sera zinazohusiana, utaratibu na udhibiti, ulioanzishwa na kutunzwa kwa mujibu wa Sheria hii;

(f) utahakikisha kwamba waajiriwa wanaohusika wanapewa mafunzo stahiki mara kwa mara katika utambuzi na usimamizi wa miamala shuku inayohusiana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi;

(g) utaweka utaratibu wa kufuatilia utekelezaji kwa kuhakikisha kwamba afisa mfuatialiaji katika ngazi ya uongozi anateuliwa; na

(h) utahakikisha ukaguzi huru na wa mara kwa mara wa sera za ndani, taratibu na udhibiti uliowekwa chini ya kifungu hiki unafanyiwa kazi.

(2) Katika kuamua, iwapo mtu amefuata sharti lolote la aya ya (e) na (f) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mahakama itazingatia mazingira yote ya kesi, ikijumuisha mila na mifano bora ambayo inayoweza kuendana na wakati katika biashara husika, shughuli, taaluma au ajira, na inaweza kuzingatia mwongozo wowote husika uliopitishwa au kuidhinishwa na mamlaka ya umma au chombo chengine kinachosimamia, kudhibiti au ni mwakilishi wa biashara, shughuli, taaluma au ajira inayofanywa na mtu huyo.

10. Kifungu cha 14 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa: Marekebisho ya Kifungu cha 14.

(a) kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kipya kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Pamoja na masharti ya kifungu cha 13 cha Sheria hii, mtoa taarifa:

(a) kwa upande wa watoa taarifa wenye miundo ya ushirika wa vikundi, wataandaa na kutekeleza programu endelevu za vikundi kwa ajili ya kukabiliana na

utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi, kama ilivyoainisha katika kifungu cha 13, ambapo inajumuisha sera, taratibu na udhibiti kwa ajili ya kubadilishana taarifa ndani ya kikundi;

(b) kwa upande wa watoa taarifa ambao muundo wa taasisi yao unafanya kazi nje ya mipaka ya Zanzibar, watahakikisha kwamba matawi ya nje ya Zanzibar na umiliki wa hisa nyingi katika kampuni tanzu wanatumia njia za kupambana utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 13 cha Sheria hii;

(c) kwa upande wa shughuli za nje za watoa taarifa, endapo masharti ya chini ya kukabiliana utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi ya nchi mwenyeji au mamlaka yenye vikwazo vyepesi kuliko vile vya Zanzibar, mtoa taarifa atahakikisha kwamba matawi yao na umiliki wa hisa nyingi katika kampuni tanzu ndani ya nchi mwenyeji wanatekeleza masharti ya Zanzibar kwa kiwango ambacho sheria ya nchi mwenyeji inaruhusu;

(d) endapo nchi mwenyeji hairuhusu utekelezaji bora wa njia za Zanzibar, watoa taarifa watatumia njia bora za ziada kusimamia viashiria hatarishi vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi na kuzijuilisha taasisi za usimamizi katika nchi mwenyeji au mamlaka, na Zanzibar; na

(e) endapo njia za ziada hazitoshelezi, taasisi husika ya usimamizi ya Zanzibar itazingatia hatua za ziada za usimamizi ikijumuisha kuweka udhibiti wa ziada kwa mtoa taarifa ikijumuisha kama itakavyofaa kulitaka kundi la kifedha kufunga shughuli zake katika nchi mwenyeji au mamlaka.

(b) kufuta kifungu kidogo cha (4).

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 14A.

11. Kifungu cha 14A cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 14A kama ifuatavyo:

"Adhabu za kiutawala.

14A. Endapo mtoa taarifa atashindwa kufuata masharti ya kutoa taarifa yaliyowekwa chini ya kifungu cha 10,10C,11,12,13 na 14 vya Sheria hii, FIU au taasisi ya usimamizi kama itakavyokuwa itatoa adhabu za kiutawala dhidi ya mtu huyo kama itakavyoainishwa katika kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii."

Marekebisho ya Kifungu cha 15.

12. Kifungu cha 15 Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza maneno "ametenda kosa na" baada ya maneno "kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki" yanayojitokeza katika kifungu kidogo cha (2).

Marekebisho ya kifungu cha 16.

13. Kifungu cha 16 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, katika mambo yoyote yanayohusiana na kukabiliana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi, mamlaka zenye uwezo na watoa taarifa wanaweza kubadilishana taarifa baina yao na wenzao nje ya nchi."

Marekebisho ya kifungu cha 17.

14. Kifungu cha 17 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "benki, muuza fedha taslim au taasisi ya fedha, taasisi maalum isiyofanya biashara ya kifedha, au mtaalum au wakurugenzi wao, mkuu wa taasisi, washirika, wataalamu au waajiriwa" yanayoonekana katika kifungu hicho na kuweka maneno "mtoa taarifa, au mtu mwengine yoyote aliyeajiriwa kwa njia yoyote au aliyehusishwa na mtoa taarifa."

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 18.

15. Kifungu cha 18 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 18 kama ifuatavyo:

"Wajibu wa kuripoti fedha taslim zinazovushwa mipaka.

18.-(1) Mtu yeyote anayesafirisha au anayetaka kusafirisha au ambaye kasafirisha kuingia au kutoka Zanzibar fedha taslimu au hati ya malipo kiwango chochote sawa na, au zaidi ya kiasi kilichowekwa na Waziri, atatoa taarifa ya kiwango cha fedha taslimu hizo au hati ya malipo kwa mamlaka za forodha, ambazo watahakikisha taarifa hizo na kuziwasilisha FIU.

(2) Afisa Forodha atakuwa na mamlaka ya kuhoji juu ya fedha taslimu au hati ya malipo kutoka mtu anayetoa taarifa, endapo kutakuwa na sababu za msingi za kushuku za kutokutoa taarifa, taarifa za uwongo au zisizo sahihi, au kushuku kutendeka kwa kosa la utakatishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi, ufadhili wa silaha za maangamizi au kosa tangulizi.

(3) Endapo afisa forodha ataridhika kwamba:

(a) kiwango chochote cha fedha taslimu au hati ya malipo ya mmiliki haijatolewa taarifa;

(b) kiwango chochote cha fedha taslimu au hati ya malipo ya mmiliki au taarifa nyengine yoyote, au maelezo au taarifa zisizosahihi au taarifa zisizojitosheleza zimetolewa;

(c) mtu anayetoa taarifa hajatoa maelezo ya kuridhisha au ya kujitosheleza kuhusu, miongoni mwa mambo mengine, chanzo cha fedha taslimu au hati ya malipo, wanufaika wa mwisho, au matumizi yaliyokusudiwa ya fedha taslimu au hati ya malipo ya mmiliki; au

(d) kuna tuhuma ya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi, ufadhili wa silaha za maangamizi au kosa tangulizi, hata kama fedha taslimu au hati za malipo za mmiliki zimetolewa taarifa kwa uhakika au kwa usahihi,

atasimamisha, kuzuia au kukamata kiasi chote cha fedha taslimu au hati za malipo za mmiliki kinachohitaji kutolewa taarifa au sehemu ya fedha taslimu au hati za malipo za mmiliki kwa namna itakavyoelezwa katika Kanuni.

(4) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atapewa adhabu za:

(a) kiutawala kwa mujibu wa Kanuni za Sheria hii; au

(b) jinai kwa mujibu wa kifungu cha 81B cha Sheria hii, na kwa kuengezea, mahakama inaweza kuamuru kutaifishwa kwa fedha taslimu au hati ya malipo ya mmiliki kwa kosa lililotendwa.”

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 18A.

16. Kifungu cha 18A cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 18A kama ifuatavyo:

“Majukumu ya FIU na taasisi ya usimamizi.

18A.-(1) FIU au taasisi ya usimamizi:

(a) itasimamia watoa taarifa ili watekeleze masharti ya Sheria hii;

(b) itafanya uchunguzi wa ndani na nje kwa lengo la ufuatiliaji na kuhakikisha watoa taarifa wanafuata masharti; na

(c) itatoa adhabu za kiutawala kwa watoa taarifa kwa ukiukwaji wa masharti.

(2) Kwa mujibu wa aya ya (b) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, usimamizi wa kukabiliana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi utajumuisha usimamizi au ufuatiliaji wa matumizi ya kundi jumuishi.

Kufuta na kuweka badala yake kichwa cha habar kipya cha Sehemu ya IV.

17. Kichwa cha habari cha Sehemu ya IV cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kichwa cha habari kipya kama ifuatavyo:

"SEHEMU YA IV
UCHUKUAJI NA UTAIFISHAJI"

Marekebisho ya Kifungu cha 19.

18. Kifungu cha 19 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza aya mpya ya (b) mara baada ya aya ya (a) katika kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(b) amri ya kuchukua mali yoyote yenye thamani inayolingana; au"

(b) kuipa nambari upya aya ya (b) kwenye kifungu kidogo cha (1) kuwa aya ya (c);

(c) kuongeza kifungu kidogo cha (6) mara baada ya kifungu kidogo cha (5) kama ifuatavyo:

"(6) Muda uliotolewa wa kutuma maombi katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki unaweza kuongezwa na mahkama endapo kutakuwa na sababu za msingi za kuongezwa muda huo".

Marekebisho ya kifungu cha 20.

19. Kifungu cha 20 Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuingiza maneno "ndani ya siku thelathini" baina ya maneno "atatoa" na "indhari ya maandishi" yanayojitokeza katika aya ya (a) ya kifungu kidogo cha (1);

(b) kuingiza maneno "ambaye anaonekana kuwa na maslahi kwenye mali" baina ya maneno "watu" na "ndani" yanayojitokeza katika aya ya (c) ya kifungu kidogo (1); na

(c) kuingiza maneno "ndani ya siku thelathini" baina ya maneno "atatoa" na "indhari ya maandishi" yanayojitokeza katika aya ya (a) ya kifungu kidogo cha (2).

Marekebisho ya kifungu cha 21.

20. Kifungu cha 21 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuingiza maneno "ndani ya siku kumi na nne" baina ya maneno "atatoa" na "indhari ya maandishi" yanayojitokeza katika aya ya (a) ya kifungu kidogo cha (3); na

(b) kuingiza maneno “ndani ya siku kumi na nne” baina ya maneno “atatoa” na “mtu” yanayojitokeza kifungu kidogo cha (4).

Kuongeza kifungu kipya cha 23A.

21. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 23A mara baada ya kifungu cha 23 kama ifuatavyo:

“Amri ya kutaifisha pale mtu anapo-fariki.

23A.-(1) Endapo mtu atafariki dunia wakati upelelezi unaendelea au baada ya kufunguliwa mashtaka kabla ya kutiwa hatiani, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuiomba mahkama kutoa amri ya kutaifishwa na kutangaza kwa umma.

(2) Mahkama inaweza kulikubali ombi la amri ya kutaifisha, endapo itaridhika kwa kuzingatia uwiano wa matokeo, kwamba:

(a) mtu alikuwa katika upelelezi wakati anafariki na hatua muafaka zilichukuliwa katika kufanya upelelezi kwa kosa linalodaiwa kutendeka; au

(b) mtu ameshtakiwa lakini akafariki kabla ya kumalizika kwa kesi, na kuna sababu za msingi za kuamini kwamba amri ya kutaifisha mali ingeweza kutolewa dhidi yake iwapo angelikuwa hai.

(3) Endapo Mkurugenzi wa Mashtaka anapeleka ombi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kwa ajili ya amri ya utaifishaji wa mali:

(a) atatoa indhari ya maandishi ya ombi kwa mtu au mtu mwengine yeyote kwamba anasababu ya kuamini ana maslahi katika mali hiyo;

(b) mtu huyo, na mtu mwengine yeyote anayedai maslahi katika mali, anaweza kujitokeza na kutoa ushahidi wakati wa usikilizaji wa ombi; na

(c) mahkama, inaweza wakati wowote kabla ya maamuzi ya mwisho ya ombi, kumuelekeza Mkurugenzi wa Mashtaka kutoa indhari ya ombi kwa mtu maalum au aina ya watu katika namna na ndani ya muda uliowekwa kama mahkama itakavyoona inafaa.”

Kuongeza vifungu vipya vya 24A na 24B.

22. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 24A na 24B mara baada ya kifungu cha 24 kama ifuatavyo:

“Kuchukua mali yenye thamani sawa.

24A.-(1) Endapo mali inayolengwa kuchukuliwa:

(a) haiwezi kupatikana hata baada ya kufanya uchunguzi;

(b) imehamishwa au kuuzwa kwa mtu mwengine ambaye wakati wa kupokea au kununua mali hiyo hakuwa na taarifa kwamba imeuzwa kwa lengo la kuepuka kufunguliwa mashtaka au kutaifishwa;

(c) imepelekwa nje ya nchi na haiwezi kupatikana tena;

(d) imepunguzwa thamani kwa kiasi kikubwa; au

(e) imechanganywa na mali nyengine kiasi kwamba inakuwa vigumu kuitofautisha,

mahkama inaweza kuamuru kuchukuliwa mali nyengine yoyote ya mtu aliyetiwa hatiani yenye thamani sawa na mali inayolengwa kuchukuliwa."

"Kutengua uhamisho wa umiliki wa mali.

24B.-(1) Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuiomba mahkama kutoa amri ya kutengua uhamishaji au uhaulishaji wowote wa mali endapo atakuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba mali imeondoshwa kuepuka kuchukuliwa.

(2) Mahkama inaweza, kabla ya kutoa amri ya kuchukuwa, kwa upande wa mali inayohusiana na amri ya kuzuia iliyotolewa, na indhari yake imetolewa kwa mujibu wa Sheria hii, itategua uhamishaji au uhaulishaji wa mali, maslahi ambayo yanayotokana na mazingira ambayo yanapelekea kuwepo kwa sababu za msingi kwamba mali hiyo imehaulishwa kwa madhumuni ya kuepuka amri ya kuchukuwa.

(3) Masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hayatatumika endapo uhamishaji au uhaulishaji umefanywa kwa thamani inayojitosheleza kwa mtu ambaye anafanya jambo hilo kwa nia njema na bila ya kuwa na taarifa."

Marekebisho ya kifungu cha 26.

23. Kifungu cha 26 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza maneno "isipokuwa kwa idhini ya Mahkama" baada ya neno "kifungu" mwishoni mwa kifungu kidogo cha (3).

Marekebisho ya kifungu cha 27.

24. Kifungu cha 27 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "haraka iwezekanavyo" yanayojitokeza mwanzoni mwa aya ya (a) katika kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake maneno "ndani ya siku kumi na nne".

Marekebisho ya kifungu cha 32.

25. Kifungu cha 32 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

"(5) Dhana ya kifungu kidogo cha (4) haitatenguliwa kwa sababu tu ya kusema kwamba mali hiyo imepatikana kutokana na kosa ambalo halijafunguliwa mashtaka."

(b) kuvipa nambari upya vifungu vidogo vilivyobakia kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 33.

26. Kifungu cha 33 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza aya mpya ya (b) mara baada ya aya ya (a) ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(b) amana yoyote au chombo chengine chochote kilichosajiliwa ambacho kina uhusiano na au chenye maslahi katika mali;"

(b) kuipa namba aya ya (b) kuwa aya ya (c).

Marekebisho ya kifungu cha 35.

27. Kifungu cha 35 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "kifungu cha 40(4)" yanayojitokeza baina ya maneno "kwa" na "ya" katika kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake maneno "kifungu cha 53(4)".

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 40.

28. Kifungu cha 40 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 40 kama ifuatavyo:

"Kuchukuliwa kwa mali ambapo mtuhumiwa hawezi kufikishwa mahkamani.

40.-(1) Endapo Mkurugenzi wa Mashtaka anashuku kuwepo sababu za msingi kwamba mtu yeyote amepata, anashikilia au anajishughulisha na mali iliyotokana na uhalifu na hakuna uwezekano wa:

(a) kumfikisha mtu mahkamani kwa kosa lolote kubwa; au

(b) kuomba amri ya adhabu ya fedha ya kigeni au amri ya kigeni ya kuchukuwa dhidi ya mtu huyo,

Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuiomba Mahkama Kuu kutoa amri ya kutangaza kuchukuliwa mali husika na kuwa ya Serikali.

(2) Mkurugenzi wa Mashtaka atawataja kuwa ni wadaiwa katika ombi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki wale ambao tu wanamiliki, wanazo au wanadhibiti mali iliyotokana na uhalifu.

(3) Utaratibu wa kutoa indhari ulioainishwa chini ya kifungu cha 20 cha Sheria hii, utatumika sawa katika ombi litakalofanywa chini ya kifungu hiki.

(4) Endapo Mahakama Kuu itaridhika kwamba mali inayotokana na uhalifu ambayo inahusika na ombi, ni mali iliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mahakama itaamuru mali hiyo ichukuliwe na kuwa mali ya Serikali.

(5) Endapo mahkama itakataa ombi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mahkama itatoa amri inayoielezea mali na kutoa tamko kwamba mali hiyo si mali iliyoainishwa katika kifungu kidogo hicho.

(6) Endapo mahkama itaridhika kwamba mmiliki wa mali iliyotokana na uhalifu iliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki:

(a) ana maslahi katika mali ambayo inahusika katika ombi; na

(b) amechukua tahadhari za kutosha kuhakikisha kuwa mali hiyo haihusiki na uhalifu,

Mahkama itatoa amri ya kwamba maslahi yasiathiriwe na amri ya kuchukua.

(7) Mtu anayedai maslahi katika mali iliyochukuliwa na ambaye hakupewa indhari chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, anaweza kuwasilisha ombi Mahkama Kuu kubadilisha au kutengua amri iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, si zaidi ya siku sitini baada ya siku ambayo amri ya kuchukuwa ilipotolewa.

Kuongeza vifungu vipya vya 41A na 41B.

29. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 41A na 41B mara baada ya kifungu cha 41 kama ifuatavyo:

"Kukusanya taarifa au nyaraka zinazohusiana na mali.

41A.-(1) Kwa madhumuni ya kukusanya taarifa zinazohusiana na mali chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote, afisa mpelelezi anaweza kumuita, kumuhoji na kuweka kumbukumbu ya maelezo ya mtu yeyote mwenye taarifa au nyaraka zinazohusiana na mali.

(2) Mtu yeyote ambaye atashindwa bila ya kuwa na sababu za msingi kufika mbele ya afisa mpepelezi kwa ajili ya kuhojiwa au kutoa nyaraka au kitu chengine chochote kinachohusiana na uchunguzi wa mali chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, au kuwa shahidi katika uchunguzi huo akakataa kujibu swali lolote aliloulizwa au kutoa nyaraka yoyote au kitu chengine chochote kinachohusiana na uchunguzi, ametenda kosa, na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote viwili."

"Kutoa taarifa za upepelezi.

41B.-(1) Mtu yeyote atakayetoa taarifa kwa mtuhumiwa au mtu mwengine asiyeidhinishwa, taarifa zinazohusiana na uchunguzi unaoendelea au kusitishwa chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote kwa nia ya kuingilia au kuvuruga uchunguzi ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania au kifungo cha kipindi kisichopungua miaka mitano au vyote viwili.

(2) Endapo mtu anayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki ni chombo kinachojitegemea, mtu huyo atalipa faini isiyopungua Shilingi Million Mia Tano za Kitanzania au mara tatu ya thamani ya mali inayochunguzwa, yoyote iliyo kubwa."

Marekebisho ya kifungu cha 42.

30. Kifungu cha 42 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta neno "mali" baada ya maneno "hakimu kwa ajili ya" yanayojitokeza katika kifungu kidogo cha (1)cha kifungu hiki.

Marekebisho ya kifungu cha 44.

31. Kifungu cha 44 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "kutafuta katika kituo" baina ya maneno "au" na "juu" na kuweka badala yake neno "kuingia".

Marekebisho ya kifungu cha 47.

32. Kifungu cha 47 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kubadilisha maneno "kosa maalum la kigeni" yanayojitokeza katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, na popote pale yatakapojitokeza katika Sheria hii na kusomeka "kosa kubwa la kigeni".

(b) kufuta maneno "Mkuu wa Jeshi la Polisi" yanayojitokeza katika kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, na kuweka badala yake maneno "Kamishna wa Polisi au wakuu wa mamlaka nyengine za uchunguzi";

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 48.

33. Kifungu cha 48 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 48:

"Amri za kuzuia.

48.-(1) Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuwasilisha ombi la kusikiliza upande mmoja mahkamani kwa ajili ya amri ya kuzuia mali ya mtu ambaye:

(a) anachunguzwa, na ameshtakiwa au ametiwa hatiani kwa kosa kubwa ikiwemo mali ya mtu asiyekuwa mtu ambae yupo chini ya uchunguzi au ameshtakiwa na au ametiwa hatiani kwa kosa kubwa; au

(b) hawezi kufikishwa mahkamani lakini mali yake inahusika katika kuchukuliwa chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote ikijumuisha mali ya mtu

mwengine yeyote ambayo ana maslahi au mali ambayo ipo chini ya udhibiti wake au maelekezo yake.

(2) Kwa ombi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mahkama inaweza, kwa kuzingatia kifungu cha 49 cha Sheria hii:

(a) kutoa amri kwamba mali iliyoainishwa katika ombi isiondoshwe au vyenginevyo isishughulikiwe, na mtu yeyote isipokuwa kwa namna na kwa mazingira yaliyoainishwa katika amri;

(b) ikiwa Mahkama itajiridhisha na mazingira yanayohitajika, itaelekeza kwamba mali hiyo au sehemu ya mali hiyo kama ilivyoelezwa katika amri, iwekwe chini ya uangalizi na kuhifadhiwa na mdhamini atakayeteuliwa na Mahkama kwa madhumuni hayo; au

(c) kuamrisha Msimamizi Mkuu au mdhamini mwengine yeyote wa umma kuangalia na kutunza mali iliyozuiliwa.

(3) Amri ya kuzuia mali ya mtu inaweza kutolewa kulingana na masharti ambayo Mahkama itaona inafaa na inaweza kuweka masharti ya kuwezesha kupatikana katika mali hiyo:

(a) gharama za kawaida za maisha ya mtu huyo;

(b) gharama za matumizi za watu wanaomtegemea na gharama za kawaida za biashara;

(c) gharama za kawaida za mtu huyo katika utetezi wa kesi ya jinai; na

(d) deni maalum aliloingia mtu huyo akiwa na nia njema, ambalo ni deni lisilokuwepo katika aya ya (a) wala aya (b).

(4) Mahkama haitoweka masharti lolote lililoainishwa katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, isipokuwa imejiridhisha kwamba mdaiwa hawezi kufikia matumizi au kulipa deni linalotokana na mali ambalo halihusiki na kizuizi.

(5) Endapo mdhamini atachukua dhamana ya mali yoyote kwa mujibu wa kifungu hiki, anaweza kufanya jambo lolote kwa madhumuni ya kutunza mali, ikijumuisha:

(a) kuwa mdaawa katika kesi yoyote ya madai inayoathiri mali hiyo;

(b) kuhakikisha mali imewekewa bima; na

(c) ikiwa mali inajumuisha, sehemu ya mali au mali yote ya biashara, kuajiri au kusitisha ajira za watu katika biashara hiyo.

(6) Katika kumteuwa mdhamini kwa mujibu wa aya ya (b) ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Mahkama itazingatia sifa za mdhamini wa mali ambayo ipo chini amri ya kuzuia.

(7) Pamoja na amri iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Mahkama inaweza kutoa amri:

(a) kuondosha mali iliyo chini ya zuio ambayo inaharibika, kuchakaa au kupungua thamani kadiri muda unavyopita, au matengenezo yake yanaweza kusababisha gharama kubwa;

(b) mapato yatokanayo na mali iliyoondoshwa yawekwe katika akaunti maalum ya usimamizi wa muda mpaka ombi la kuchukua litakapofika mwisho au mahkama itakavyoamuru vyenginevyo.

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 49.

34. Kifungu cha 49 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 49 kama ifuatavyo:

"Sababu za kutoa amri ya zuio.

49.-(1) Endapo ombi la amri ya zuio limefanywa dhidi ya mali, Mahkama kwa kuzingatia kifungu hiki, itatoa amri ya kuzuia dhidi ya mali hiyo.

(2) Endapo ombi limefanywa kabla ya mtu kufunguliwa mashtaka, mahkama haitatoa amri ya zuio isipokuwa ikijiridhisha, kwa kuzingatia mambo yaliyomo katika hati ya kiapo, kwamba hatua stahiki zimechukuliwa kuchunguza kosa na upo uwezekano wa mtu huyo kufunguliwa mashtaka kwa kosa hilo.

(3) Endapo mdaiwa hajatiwa hatiani, Mahkama haitatoa amri ya zuio isipokuwa ikijiridhisha kwamba:

(a) zipo sababu za msingi za kuamini kwamba mdaiwa ametenda kosa; na

(b) mali hiyo imetokana na uhalifu au mtuhumiwa alinufaika kutokana na kutenda kosa hilo.

(4) Endapo mdaiwa atatiwa hatiani, mahkama haitatoa amri ya zuio mpaka:

(a) itakaporidhika kwamba mdaiwa ametiwa hatiani kwa kosa kubwa; na

(b) mdaiwa amenufaika moja kwa moja au vyenginevyo kutokana na kutendeka kwa kosa hilo.

(5) Endapo amri ya zuio imeombwa dhidi ya mali ya mtu mwengine ambaye si mdaiwa, mahkama haitatoa amri ya zuio isipokuwa kama kuna sababu za msingi za kuamini kwamba:

(a) mali hiyo imetokana na uhalifu; au

(b) mdaiwa ana maslahi katika mali hiyo au mali hiyo iko chini ya udhibiti au maelekezo ya mdaiwa, ambaye alinufaika moja kwa moja au vyenginevyo kutokana na kufanyika kwa kosa kubwa.

(6) Endapo amri ya zuio imeombwa dhidi ya mali ya mtu ambaye hawezi kufikishwa mahkamani, mahkama haitatoa amri ya zuio isipokuwa kama zipo sababu za msingi za kuamini kwamba mali hiyo itachukuliwa chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote.

(7) Amri ya zuio itatolewa dhidi ya mali endapo kuna hatari ya mali hiyo kuondoshwa au imeshughulikiwa kwa namna yoyote ile ambayo ingepelekea kuziua zoezi la uchukuwaji wowote, au amri ya adhabu ya faini kuhusiana na mali hiyo kwa mujibu wa Sheria hii.

(8) Amri ya zuio iliyotolewa kabla ya kufunguliwa kwa mashtaka chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, itafanyakazi kwa muda wa miezi kumi na mbili, isipokuwa mahkama inaweza kuongeza muda wa kipindi cha miezi kumi na mbili baada ya ombi kuwasilishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

(9) Endapo mtu kafunguliwa mashtaka, ndani ya kipindi cha miezi sita au kama muda umeongezwa, amri ya zuio itaendelea kutekelezwa hadi itakapomaliza muda wake kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 62 cha Sheria hii.

(10) Ombi la amri ya zuio litaambatanishwa na hati ya kiapo cha mpelelezi akieleza sababu za msingi za kuamini kwake chini ya vifungu vidogo vya (2), (3) na (4) vya kifungu hiki.

Marekebisho ya kifungu cha 52.

35. Kifungu cha 52 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) Mtu yeyote aliyeathirika kutokana na amri ya zuio anaweza, ndani ya siku kumi na nne baada ya kupewa indhari ya zuio hilo, kuomba mahkama kubadilisha au kufuta amri ya zuio au amri nyengine yoyote ambayo Mahakama inaweza kutoa chini ya kifungu cha 53 cha Sheria hii."

Marekebisho ya kifungu cha 53.

36. Kifungu cha 53 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (3) kama ifuatavyo:

"(3) Mahakama inaweza, kwa maombi ya mtu aliyeathirika kutokana na amri ya zuio, kubadilisha au kufuta amri ya zuio endapo itaridhika kwamba:

(a) mali husika haitokani na uhalifu; au

(b) maslahi katika mali hiyo yalipatikana kwa thamani halisi ya mali hiyo, bila kujua, na katika mazingira ambayo hayapelekei kuwepo kwa tuhuma kwamba mali hiyo ilitokana na uhalifu.

Marekebisho ya kifungu cha 60.

37. Kifungu cha 60 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza maneno "sifa, usimamizi," baina ya maneno "mshahara" na "na" yanayojitokeza katika kifungu kidogo cha (2).

Kufutwa kwa kifungu cha 66.

38. Kifungu cha 66 cha Sheria Mama kinafutwa.

Kuongeza kifungu kipya cha 72A.

39. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 72A mara baada ya kifungu cha 72 kama ifuatavyo:

"Kutoa taarifa kuhusu mali.

72A.-(1) Afisa upelelezi anaweza, kwa indhari ya maandishi, ndani ya muda na kwa namna itakavyoainishwa katika indhari, kumtaka mtu yeyote anayechunguzwa au anayeshukiwa kutenda kosa kubwa, atoe maelezo kamili na ya kweli ya mali yote au sehemu ya mali ambayo mtu huyo:

(a) anamiliki, anadhibiti, anaisimamia au ananufaika nayo; au

(b) alimiliki, aliidhibiti, aliisimamia au ana haki ya kunufaika nayo.

(2) Mtu anayetakiwa kutoa taarifa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, anaweza, pamoja na taarifa iliyoombwa, kutoa maelezo ya kina ya msingi ya kuonesha kwamba mali hiyo haitokani na shughuli za kihalifu.

(3) Mtu anayetoa maelezo kutokana na ombi la kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atatoa taarifa inayohitajika kwa afisa uchunguzi ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya agizo, isipokuwa kama atatoa maelezo ya kumridhisha afisa uchunguzi kwamba aongezewe muda wa kutekeleza agizo hilo.

(4) Katika ombi lolote la amri ya kutaifisha chini ya Sheria hii, majibu ya agizo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki yanaweza kukubaliwa kama ushahidi katika shauri la kutaifisha.

(5) Mtu ambaye katika kutekeleza agizo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, akatoa taarifa za uongo ametenda kosa na akitiwa hatiani atachukuliwa hatua kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 97 cha Sheria ya Adhabu.”

Kuongeza kifungu kipya cha 78A.

40. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 78A mara baada ya kifungu cha 78 kama ifuatavyo:

“Katazo la kuzuia haki.

78A. Mtu yeyote atakayetumia nguvu, vitisho, hofu, ahadi, anatoa zawadi au fursa isiyostahili kwa ajili ya:

(a) kutoa ushahidi wa uongo;

(b) kuingilia utoaji wa ushahidi au uwasilishaji wa ushahidi katika shauri; au

(c) kuingilia utekelezaji wa majukumu ya hakimu, jaji, mwendesha mashtaka wa umma, wakili wa serikali au afisa yeyote anayetekeleza Sheria hii,

ametenda kosa na akitiwa hatiani atapata adhabu ya kifungo kisichopungua miaka mitano.”

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 82.

41. Kifungu cha 82 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 82 kama ifuatavyo:

“Rufaa.

82.-(1) Mtu yeyote asiyeridhika na amri ya Mahakama iliyotolewa chini ya Sheria hii anaweza kukata rufaa dhidi ya amri hiyo.

(2) Endapo mtu ameamua kukata rufaa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utekelezaji wa amri utasitishwa hadi rufaa hiyo itakapoamuliwa.

(3) Rufaa chini ya Sheria hii itaongozwa kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.”

Marekebisho ya kifungu cha 85.

42. Kifungu cha 85 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta maneno “ofisa wa polisi mwenye cheo cha mrakibu msaidizi wa polisi” na kuweka badala yake maneno “afisa mpelelezi”.

(b) kuongeza aya mpya ya (e) mara baada ya aya ya (d) kama ifuatavyo:

“(e) tumia mbinu za uwasilishaji zilizodhibitiwa.”

Kuongeza kifungu kipya cha 86A.

43. Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 86A mara to baada ya kifungu cha 86 kama ifuatavyo:

"Mamlaka ya mahakama juu ya mgeni.

86A.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Msaada wa pamoja, Mahkama Kuu itakuwa na mamlaka ya kusikiliza mashtaka yanayomhusu mtu kutoka nchi ya kigeni kwa kosa lililotendwa nje ya Zanzibar, ambalo lingekuwa ni kosa chini ya Sheria hii.

(2) Mtu kutoka nchi ya kigeni hatashtakiwa isipokuwa kwa idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mashtaka dhidi ya mtu aliyetenda kosa nje ya Zanzibar yataendeshwa endapo mtu huyo hawezi kurejeshwa katika nchi ya kigeni ambako kosa hilo lilitendeka."

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu wa marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mapato yatokanayo na Uhalifu Nam. 10 ya Mwaka 2009, ni kuondoa upungufu uliyopo katika Sheria hiyo. Kutokana na matokeo yalioainishwa katika Ripoti ya Tathmini ya Mifumo ya Nchi ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi ya Mwaka 2021, Tanzania ilionekana kuwa na upungufu katika mifumo ya udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.

Hali hiyo imepelekea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwekwa chini ya uangalizi wa FATF kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Juni, 2021 hadi Juni, 2022, ili irekebishe udhaifu uliobainishwa, ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya sheria zenye upungufu, ikiwemo Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu Nam. 10 ya Mwaka 2009.

Mswada huu umegawika katika Sehemu mbili kama ifuatavyo:

Sehemu ya Kwanza: Sehemu hii imeainisha masharti ya awali ambayo ni Jina la Mswada na kuanza kutumika, na kusomeka kwa sheria.

Sehemu ya Pili: Sehemu hii inajumuisha marekebisho kutoka kifungu cha 3 mpaka cha 46 ambayo yanajumuisha, tathmini ya viashiria hatarishi, njia za kupunguza vihatarishi na kutenga rasilimali; kumtambua mmiliki mnufaika, kutambua mteja, kuanzisha na kutunza kumbukumbu na taratibu za ndani za kuripoti; majukumu ya taasisi za usimamizi na FIU; amri ya kutaifisha, kuchukua na kuzuia.

ZANZIBAR
2 Februari, 2022

(JAMAL KASSIM ALI)
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS,
FEDHA NA MIPANGO
ZANZIBAR.

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR - 2022